# Miaka mitatu ya uongozi wa Dk Samia iliyojaa neema tele kwa watumiaji wa huduma za anga nchini

Jafari Juma, Mwananchi

Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania imeendelea kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya huduma za anga.

Hii ni utekelezaji ahadi yake ambayo aliitoa wakati akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuapishwa kuingia madarakani.

"Kuhusu usafiri wa anga, Serikali itaendelea na maboresho ya viwanja vya ndege kwa kusoma mwenendo wa biashara hii ulimwenguni na kuepuka mambo yote yasiyo na tija," alisema Dk Samia.

Ni dhahiri, ahadi hii pamoja na nyingine zilizopo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 - 2025 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) zimetekelezwa kwa kiasi kikubwa na Serikali chini ya uongozi wa Dk Samia.

Serikali imetenga na kutoa fedha za kugharamia kazi kubwa inayoendelea ya upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Kigoma (Sh 40 bilioni), Mwanza (Sh 11 bilioni), Pemba (Sh 428.7 bilioni), Shinyanga (Sh 44.8 bilioni), Songea (Sh 37 bilioni), Songwe (Sh 33 bilioni), Sumbawanga na Tabora.

Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma utakaogharimu zaidi ya Sh 600 bilioni umeanza, kazi hiyo ikifanywa na mkandarasi Sinohydro & Beijing Construction Engineering ya China. Tayari zaidi ya Sh 15.2 bilioni zimetumika kulipa fidia wananchi waliopisha maeneo kwa ajili ya mradi.

Mradi huo unahusisha ujenzi wa jengo la abiria na barabara ya kutua na kuruka ndege yenye urefu wa kilomita 3.6. Baada ya ujenzi kukamilika Kiwanja hicho kitakua na uwezo wa kuhudumia abiria zaidi ya milioni 1.5 kwa mwaka.

Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa njia za kutua na kuruka ndege katika viwanja vya ndege vya Iringa (Sh 63.7 bilioni), Moshi (Sh 12.344 bilioni), Musoma (Sh 35 bilioni) na upembuzi yakinifu uliofanyika kwa ajili ya ukarabati, upanuzi na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Lake Manyara, Lindi, Njombe, Simiyu, Singida na Tanga.

Ikumbukwe msongamano wa abiria katika viwanja vya ndege pamoja na kukosekana kwa huduma zinazokidhi viwango vya kimataifa ilikuwa ni kilio cha muda mrefu cha watumiaji wa huduma za usafiri wa anga, ambacho sasa chini ya Serikali ya awamu ya sita changamoto hizo zinaendelea kutatuliwa kwa kasi kubwa.



Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan.

**"Ndani ya miaka mitatu, yaliyofanyika ni mengi sana ambapo kurasa moja pekee ya gazeti haitoshi kabisa kuyaelezea yote. Zaidi, tunapongeza jitihada za Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuonesha dhamira ya dhati ya kuboresha sekta ya usafiri wa anga."**

Innocent Kyara, Katibu Mtendaji wa TCAA CCC.

Ni chini ya uongozi wa Dk Samia, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kimekabidhiwa rasmi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kutoka kwa Kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO).

Hatua hii ni utekelezaji wa Azimio la Bunge la Novemba 4, 2022 hivyo kuhitimisha sakata la muda mrefu linalohusisha kampuni hiyo iliyoanzishwa Machi, 2018.

Aidha, pamoja na mabadiliko ya uendeshaji wa KIA, kwa kuzingatia miongozo na kanuni za kimataifa za usafiri wa anga, huduma zimeendelea kutolewa bila ya usumbufu wowote kwa watumiaji wa kiwanja hicho.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), kumekuwa na ongezeko la wataalamu, mathalani marubani (kutoka 234 hadi 603), wakaguzi wa ndege (kutoka 28 hadi 44), waongoza ndege kwenye minara (kutoka 70 hadi 154) na wataalam wa taarifa za kianga (kutoka 50 hadi 83).



Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Mwakiposa Kihenzile akipokea taarifa ya utendaji kazi kutoka kwa Katibu Mtendaji wa TCAA CCC, Innocent Kyara.

Aidha, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC). Chuo hicho kina ithibati kutoka Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) na ni miongoni mwa vyuo tisa barani Afrika vinavyotoa mafunzo ya usalama wa anga.

Kwa kuongezea, Serikali imenunua ndege mbili za mafunzo ya urubani kwa ajili ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) huku zaidi ya Sh 49 bilioni zikitengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kufundishia wataalamu wa sekta ya anga.

NIT inatoa mafunzo ya Urubani kwa daraja la awali (PPL) ambalo mwanafunzi atasoma kwa miezi sita kwa ada ya Sh 21 milioni na daraja la biashara (CPL) ambalo litachukua miezi 12 kwa ada ya Sh 53.8 milioni badala ya Sh 300 milioni kwa mafunzo hayo nje ya nchi.

Katika hatua nyingine, waziri mwenye dhamana ya Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa ameendelea kutoa ushirikiano chanya kwa taasisi zinazohusika na usimamizi na utoaji wa huduma za usafiri wa anga.

"Wizara itaendelea kujenga mazingira wezeshi kwa taasisi zilizo chini yake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Nitaendelea kuhakikisha kunakuwa na viwanja bora na miundombinu wezeshi itakayokuza biashara ya usafiri wa anga na uchukuzi kwa ujumla", alisema Profesa Mbarawa wakati wa mapokezi ya ndege mpya aina ya Boeing 737-9 Max jijini Dar es Salaam.

Kwa kutambua umuhimu wa watumiaji wa huduma za usafiri wa anga, Serikali ya awamu ya sita imeendelea kulipa ushirikiano Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Anga (TCAA CCC).

Baraza hili lilianzishwa chini ya Kifungu cha 56 cha Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 (the Civil Aviation Act, Cap 80) mahsusi kwa ajili ya kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga.

Majukumu makuu ya baraza ni kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga hapa nchini, kusambaza taarifa na maoni yenye maslahi ya watumiaji pamoja na kushirikiana na wadau wa sekta ya usafiri wa anga ikiwemo Serikali.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dk Samia, tumeshuhudia watumiaji wa huduma za usafiri wa anga wakiongezeka kutoka watumiaji 2,964,471 mwaka 2020/2021 hadi kufikia zaidi ya watumiaji 5, 723, 000,"

"Aidha, mizigo inayosafirishwa kwa njia ya anga imeongezeka kutoka tani 26,458 mwaka 2020/2021 hadi zaidi ya tani 55,000 mwaka huu. Ongezeko hili la watumiaji na kiwango cha mizigo inayosafirishwa kwa njia ya anga inatokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali, ikiwemo ununuzi wa ndege ya mizigo, hali ambayo imeongeza imani ya watumiaji katika njia hii ya usafiri na usafirishaji" anasema Innocent Kyara, Katibu Mtendaji wa TCAA CCC.

Katika utawala wa Serikali ya awamu ya sita, chini ya uongozi wa Dk Samia, mageuzi ya utumiaji wa huduma za anga hayakuishia katika sekta ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga pekee, tumeshuhudia pia matumizi ya huduma za anga yakiendelea katika maeneo na sekta nyingine.

Katika kukabiliana na changamoto ya matumizi ya vinyunyizi vya kubeba mgongoni (matabi), Serikali inayoongozwa na Dk Samia, kupitia Bodi ya Pamba (TCB), imenunua ndege 20 zisizokuwa na rubani (drone) zenye thamani ya Sh 400 milioni kwa ajili kunyunyuzia viuadudu mashamba makubwa ya pamba.




Wajumbe na Sekretarieti ya Baraza la Watumiaji Huduma za Anga (TCAA CCC) wakiwa pamoja na watumishi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) walipotembelea Kiwanja cha Ndege cha Dodoma.

**Sh 600 bilioni**

**Fedha zitakazotumika katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma.**

**20**

**Idadi ya ndege zisizokuwa na rubani ambazo zimenunuliwa na Serikali kupitia Bodi ya Pamba kwa ajili kunyunyuzia viuadudu mashamba makubwa ya pamba.**

Ndege hizo zina uwezo wa kupuliza ekari 15 hadi 20 kwa saa moja huku mkulima akipatiwa huduma hiyo bila ya gharama yoyote ya ziada.

Tanzania tuna hekta milioni 48.1 za eneo la hifadhi za misitu, usimamizi wa eneo hilo kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) pamoja na Hifadhi za Taifa unarahisishwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya ndege zisizokuwa na rubaini katika kufanya doria dhidi ya majangiri katika Hifadhi za Misitu na Wanyama.

Aidha, kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Serikali iko kwenye hatua ya kuingiza vituo vyote vya afya kuanzia zahanati hadi ngazi ya kitaifa kwenye mfumo wa kusambaza dawa kwa kutumia ndege zisizokua na rubani (drones). Utekelezaji wa mpango huu utahakikisha upatikanaji wa dawa katika vituo vya afya katika nyakati zote.

Tunapoangazia mambo makubwa yaliyofanyika katika miaka mitatu ya utawala wa Serikali ya awamu ya sita ni ngumu kuacha kuzungumzia kazi kubwa inayofanywa na Rais Dk Samia katika kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine duniani.

Mashirika ya Ndege ya Kimataifa kama Air France, Saudi Airlines, Elderweis na Eurowing ambayo yalianza kufanya safari za moja kwa moja nchini katika kipindi hiki cha uongozi wa Dk Samia ni uthibitisho wa uwepo wa mazingira sahihi ya uwekezaji katika Sekta ya usafiri wa anga na jitihada mbalimbali za kidiplomasia zinazofanywa na Serikali kuvutia wawekezaji nchini.

Safari za ndege za moja kwa moja, bila ya kuunganisha katika nchi nyingine zinapunguza muda wa safari hivyo kumuondolea uchovu mtumiaji na kumfanya afurahie safari yake.



Katibu Mtendaji wa TCAA CCC, Innocent Kyara, (wa sita kulia) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wengine kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati katika warsha iliyoandaliwa na AFCAC jijini Nairobi, Kenya.

Aidha, Agosti, 2023, Bunge liliridhia Azimio la Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga Afrika (AFCAC). Kufuatia hatua hiyo, kunaifanya Tanzania kuwa mwanachama wa AFCAC ambapo mbali na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi za Afrika, Watanzania wataweza kufaidika na fursa za uongozi na ajira zitakazojitokeza katika ICAO, AFCAC na mashirika mengine ya kimataifa ya usafiri wa anga.

Nchi yetu itashiriki na kuendeleza mipango ya pamoja katika Bara la Afrika ili kupata rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kukuza usafiri wa anga nchini, hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Kufuatia hatua hiyo, mwezi Disemba, 2023, TCAA CCC kupitia kwa Katibu Mtendaji Innocent Kyara, ilishiriki katika warsha iliyoandaliwa na AFCAC kwa taasisi za Afrika Mashariki zinazomlinda mtumiaji wa huduma za anga. Warsha hii ni mwanzo wa uhuishwaji na utengenezaji wa Sheria na Kanuni za kumlinda mtumiaji wa huduma za anga kwa Afrika nzima.

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuwa kinara wa kutafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali wanazokutana nazo watumiaji wa huduma za anga. Mathalani, ilipotokea tukio la kusikitisha la ajali ya ndege yenye usajili namba 5H-PWF, aina ya ATR42-500 ya Shirika la Ndege la Precision, Serikali kupitia taasisi zake mbalimbali zilishughulikia suala hilo kwa weledi mkubwa, ikiwemo kuruhusu vyombo vya uchunguzi kufanya kazi yake juu ya ajali hiyo.

TCAA CCC ilikaribisha familia za wahanga wa ajali hiyo kwa msaada wa madai ya fidia kwa mujibu wa Sheria. Aidha, tuliweza kushauri na kusaidia familia za wahanga watatu wa ajali hiyo juu ya malipo ya fidia. Hadi kufikia wakati huu hatujapokea malalamiko yoyote kuhusu malipo ya fidia kwa wahanga, jambo linaloashiria wahusika kuridhishwa na mchakato mzima ulivyofanyika.

Ikumbukwe, katika kuendana na kasi ya teknolojia ambayo imerahisisha mfumo wa ukusanyaji maoni au malalamiko ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga, mtumiaji anaweza kuwasilisha malalamiko kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa huduma za Serikali mtandao.

Mfumo wa E-Mrejesho unasaidia umma kufikia huduma mbalimbali za Serikali kupitia program tumishi (App) ambayo inapatikana App Store na Play Store. Aidha, kwa mtu asiyetumia simu janja anaweza kupata huduma ya kuwasilisha maoni au malalamiko yake kwa kupiga *152*00#.

Baraza linajivunia uwajibikaji wake kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kwa kuendelea kuwa daraja muhimu baina ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kwa upande mmoja na Serikali na Watoa huduma kwa upande mwingine.

"Ndani ya muda huu mfupi wa miaka mitatu, yaliyofanyika ni mengi sana ambapo kurasa moja pekee ya gazeti haitoshi kabisa kuyaelezea yote. Zaidi, tunapongeza jitihada za Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuonesha dhamira ya dhati ya kuboresha sekta ya usafiri wa anga na kwa niaba ya Baraza na watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kwa ujumla tunamshukuru sana Rais kwa kazi nzuri na tunamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake katika siku zijazo" anahitimisha Kyara.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga na umma kwa ujumla wanaweza kuwasiliana na Baraza la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) kwa elimu na ufafanuzi zaidi wa masuala mbalimbali kuhusu usafiri wa anga kupitia mitandao yetu ya kijamii ya Instagram (@tcaa_ccc), Mtandao X (@tcaa_ccc1) na Youtube (@TCAA_Consumer_Consultative_Council) au kupiga simu ya bure nambari 0800 110 190 au kupitia anuani iliyoainishwa hapa chini;

*Katibu Mtendaji,*
*Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC)*
*Majengo ya TBA Na. L1,*
*Kiwanja Na. 6/2,*
*Mtaa wa Kilimani,*
*Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,*
*S. L. P 12242,*
*14110 DAR ES SALAAM*